**KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA**

**TAARIFA KWA UMMA**

# MAFANIKIO YA KITUO CHA UWEKEZAJI KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2021-2022 NA MUELEKEO WA VIPAUMBELE VYA BAJETI 2022-2023

**Dar es Salaam, 17 Agosti, 2022**

Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kinapenda kuujulisha umma kuhusu Mafanikio kwa kipindi cha mwaka 2021-2022 na muelekeo wa vipaumbele vya bajeti mwaka 2022-2023.
TIC imepata mafanikio kutokana na kuimarika kwa shughuli za uratibu na utoaji wa huduma kwa wawekezaji kupitia utoaji wa huduma mahala pamoja (one stop facilitation centre) hivyo kusaidia katika ongezeko la usajili wa miradi, kuhamasisha uwekezaji na kuhudumia wawekezaji hapa nchini ambapo katika kipindi tajwa kuna mafanikio katika maeneo yafuatayo;

**Usajili wa Miradi mipya ya Uwekezaji**

**Katika kipindi cha mwezi *Juni 2021 hadi Julai 2022* jumla ya *miradi 274* imesajiliwa ikilinganishwa na *miradi 234* iliyosajiliwa katika kipindi hicho mwaka 2020/2021 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia *14.6. Miradi* iliyosajiliwa katika kipindi hicho inatarajiwa kuzalisha ajira 43,925 ukilinganisha na ajira *36,470* zilizoripotiwa kipindi hicho mwaka 2020/2021.**

Miradi hiyo ipo katika sekta za ***Viwanda, Usafirishaji Kilimo, ujenzi/majengo ya biashara, Miundombinu ya kiuchumi, Taasisi za fedha, rasilimali watu, usafirishaji, utalii na huduma*** (Service).

**UFANIKISHAJI UWEKEZAJI**

Kupitia Kituo cha Uwekezaji Serikali imeendelea kufanya maboresho ili kurahisisha na kuboresha utoaji wa huduma kwa wawekezaji nchini ikiwa ni pamoja na:

- **Kuboresha Kituo cha utoaji wa huduma za mahali pamoja *"One Stop Facilitation Centre ya TIC*"**. Taasisi 12 za serikali kwa sasa zinatoa huduma katika Kituo cha mahali pamoja. Taasisi hizo ni Wizara ya Kazi, Wizara ya Ardhi, Uhamiaji, NIDA, NEMC, TRA, BRELA, TBS, TMDA, OSHA, TANESCO na TIC yenyewe.
- Utengenezaji wa mfumo wa Dirisha la Pamoja la kuhudumia Wawekezaji la Kielektroniki Tanzania (TeIW) ambalo tunatarajia litakuwa ni suluhisho katika kurahisha upokeaji wa maombi, utoaji wa huduma za vibali, leseni na usajili kwa wawekezaji kwa haraka. Lengo la Mfumo huo ni kutumika kurahisisha mtiririko wa taarifa kati ya Taasisi zote zilizoko ndani ya Kituo yaani OSFC".
- Mfumo huu ambao umemefadhiliwa pia na Taasisi ya TIMEA utakuwa ni hazina ya taarifa zote muhimu kwa ajili ya uwekezaji kwa wadau wote wanaohitajika kuwekeza hapa nchini na utatekelezwa kwa Awamu tatu ambapo kwa kuanzia utahusisha Taasisi Saba ambazo ni TRA, BRELA, Kazi, Uhamiaji, NIDA, Ardhi na TIC.

**Utiaji Saini Mikataba ya Utekelezaji na Wawekezaji wakubwa wa kimkakati**

Miradi sita (6)kwa Pamoja ambayo inatarajia kuwekeza kiasi cha dola za Marekani **bilioni 1.10** ambapo itazalisha ajira za moja kwa moja zipatazo **28,710** na kuokoa fedha za kigeni zaidi ya dola za Marekani **bilioni moja** ambazo zingetumika kuingiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Miradi hiyo ni Pamoja na;

- ***Itracom Limited*** kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea
- ***Bagamoyo Sugar Limited*** inayojihusisha na Kilimo cha Miwa na Uzalishaji wa Sukari.
- ***Kagera Sugar Limited*** ambayo imejikita kwenye Kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari.
- ***Mtibwa Sugar Estates*** ni ya mradi wa Kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari.
- ***Knauf Gypsum Limited*** inafanya shughuli za uzalishaji wa Gypsum powder, na Gypsum board
- **Taifa Gas** ambayo inafanya shughuli za uchakataji na usindikaji wa gesi.

**UHAMASISHAJI UWEKEZAJI**

Kituo kimeendelea kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje kwa kushirikina na ofisi za kibalozi na ofisi za wakuu wa Mikoa. TIC bado imeendelea kupokea wawekezaji wenye nia ya kuwekeza nchini. Hii imetokana na Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na ujenzi wa miundombinu wezeshi kama ***barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na umeme***. Diplomasia ya uchumi pia imekuwa chachu katika kuifanya Tanzania kuwa kivutio katika kuwekeza barani Afrika.

**Uhamasishaji Uwekezaji Kutoka Nje**

- Katika kipindi cha kuanzia Juni 2021 hadi  Julai 2022 uhamasishaji uwekezaji wa nje umeendelea kufanyika kupitia makongamano ya uwekezaji yaliyofanyika Qatar, Doha na ushiriki wa TIC kwenye kongamano na maonesho haya yameleta matokeo chanya ambapo wawekezaji mbalimbali walifika nchini k
- TIC pia imeendelea kusaidia wawekezaji kwa kuandaa miradi na kuinadi kwa wawekezaji katika Forum mbalimbali ili kupata taarifa mbalimbali za uwekezaji.
- ***TIC iliandaa vikao vya Makampuni mbalimbali*** ya wawekezaji watarajiwa waliofika TIC kwa nyakati tofauti kuanzia mwezi Juni 2021 hadi Julai 2022 na kuelezwa fursa za uwekezaji pia kupewa miongozo/taratibu za uwekezaji kutoka kwenye taasisi husika. Pia wageni zaidi mbalimbali waliweza kufika katika ofisi za TIC na kupata taarifa mbali mbali za uwekezaji.
- TIC imeendelea kuhamasisha na kushiriki kuvutia uwekezaji katika uanzishwaji wa miradi mbalimbali ikiwemo uanzishwaji wa kongani za viwanda (industrial park) Kilimo, viwanda kama vile viwanda vya mbolea, madawa na vifaa tiba, uvuvi na mifugo na tayari wawekezaji wameonekana wakimiminika kuja kuchukua fursa husika. Kituo kinaendelea na kazi ya kuratibu vikosi kazi mbalimbali katika kufanikisha uwekezaji husika.
- Mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kuhamasisha Diplomasia ya Uchumi itasaidia katika kuinua na kufanikisha uhamasishaji wa Uwekezaji hapa nchini. Taswira nzuri inayofanywa kupitua ziara za Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan zinaleta sura kuwa Tanzania ni sehemu bora na inayofaa kuwekeza.

- TIC imefanya vikao na Diaspora nchini Misri na nchi za Scandinavia

**Uhamasishaji Uwekezaji wa Ndani**

- Wawekezaji wa ndani wameendelea kutembelea Kituo cha Uwekezaji kutafuta fursa.
- TIC pia imeendela kusaidia wawekezaji wa ndani kwa kuratibu uwasilishwaji wa miradi ya watanzania katika Forum mbalimbali.
- Katika kipindi cha kuanzia Juni 2021 mpaka Julai 2022 uhamasishaji uwekezaji kutoka nje umeendela. TIC imeweza kuandaa na kushiriki makongamo makubwa katika nchi za Misri (2), Kenya (1), Burundi (1), Ufaransa, Ubelgiji, Qatar, Uturuki, Afrika Kusini, Algeria na makongamano kadhaa yaliyoandaliwa Dubai kipindi cha Expo 2020 Dubai
- Kuratibu na Kushiriki makongamano ya biashara na uwekezaji kwa njia ya mtandao (virtual / online meetings) kwa kushirikina na ofisi za kibalozi / taasisi za biashara na sekta binafsi za nchini China, Japan, Nigeria, India, Qatar, Ujerumani, Canada, Pakistan, Italia, Algeria, Sweden na Vietnam

**Uboreshaji wa mifumo ya kurahisisha huduma kwa wawekezaji**

Serikali imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha inarahisisha utoaji huduma kwa kuondoa urasimu, kutumia teknolojia ya mawasiliano, na kuweka vigezo vinavyo tumika kutoa huduma kama ifuatavyo

- Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji imerahisisha mfumo wa utoaji cheti cha Uwekezaji kimefanya maboresho ya utendaji kazi wa ndani (***Business Process Engineering), mtiririko wa nyaraka na mafaili***, utoaji maamuzi wenye tija. Mwanzo mwekezaji alikuwa anapitia mtiririko wa hatua ***44, kwa sasa ni hatua 13*** mpaka kupata Cheti za Uwekezaji.
- Serikali imeweka ***vigezo na viwango vya utoaji huduma kwa wawekezaji,*** huduma zinatakiwa kwa wawekezaji ndani ya siku tatu kwa cheti cha uwekezaji, na kwa vibali vingine vyote vitoke ndani ya siku kumi na nne. Kwa vibali vyenye matatizo ya kisera serikali imeweka utaratibu wa wawekezaji wanapewa vibali vya muda (provisional licenses).

**Katika Mwaka 2022/2023, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-**

- Kuendelea kuboresha mifumo ya kusajili ili kuongeza idadi ya miradi ya uwekezaji inayosajiliwa na Kituo;
- Kuendelea kuboresha na kuimarisha huduma zitolewazo katika Kituo cha Huduma za Mahali Pamoja (One Stop Facilitation Centre) ili kufanikisha uwekezaji;
- Kuendelea na mkakati wa kufuatilia na kutathmini miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa (Project Monitoring & Evaluation);
- Kuendelea na kutafuta ardhi kwa ajili ya uwekezaji;
- Kuendelea kuhamasisha uwekezaji ndani na nje ya nchi kupitia makongamano na semina;
- Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya masuala mbalimbali ya uwekezaji nchini kupitia vyombo vya habari na mitandao; vii.Kuendelea kutatua migogoro na changamoto za uwekezaji.
- Kufanya tafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na tafiti za kuibua fursa za uwekezaji nchini, tafiti za kuboresha mazingira ya uwekezaji, tafiti za kuibua maeneo yenye fursa za uwekezaji kwa ajili ya wajasiramali wa kati na wadogo;
- Kuendelea kushirikiana na Balozi za Tanzania katika kuitangaza Tanzania ili kuvutia uwekezaji kutoka nchi zilipo balozi hizo; na
- Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Kituo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**Imetolewa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**